# OFISI RAIS
# TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
## SHULE YA SEKONDARI MAKABE

S.L.P ……………,

**SIMU: +255 755 116 945**

**DAR ES SALAAM.**

**+255 712 284 293**

**E MAIL:** makabesec2022@gmail.com

---

### FORM YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA – 2023

Uongozi wa shule ya Sekondari **MAKABE** unayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023 katika shule ya Sekondari **MAKABE** kama mwanafunzi wa **kutwa**. Hongera sana kwa kupata nafasi hii adimu.

**MAHALI SHULE ILIPO**: (eleza shule ilipo)
Shule ya sekondari **MAKABE** Ipo mkoa wa Dar es salaam, Wilaya ya Ubungo, Kata ya **MBEZI** mtaa wa **MAKABE barabara ya msumi kituo cha njia panda ya tabata** umbali kutoka barabara kuu ya Morogoro kufika shuleni ni kilometa **saba**

**MUDA WA KUFUNGUA SHULE**
Shule itafunguliwa tarehe **09/01/2023** Saa 1:00 asubuhi fika na vitu vyote vinavyohitajika ili uweze kusajiliwa. Mwanafunzi ambaye hataripoti kwa ;muda uliopangwa, nafasi yake itajazwa na mwanafunzi mwingine.

**MAHITAJI MUHIMU YAKUJA NAYO SHULENI**

1. Sare ya Shule (Imeainishwa hapo chini kwa jinsia)
2. Begi la kubebea madaftari lenye mikanda miwili la kubeba mgongoni.
3. Mkebe wa vifaa vya hisabati.
4. Madaftari 11 counter book (Quire 3 au 4). Daftari ndogo 11 za Msomi kwa ajili ya kufanyia mazoezi.
5. Kamusi (Dictionary) English to Kiswahili au English to English.
6. Mathematical four figure table.
7. Kalamu ya wino na risasi pamoja na rula.
8. **T-shirt** ya shule, **Sweta** rangi ya maruni, **track suit** ya rangi ya kijivu na mistari ya rangi nyeupe, raba nyeupe kwa ajili ya michezo.
9. Faili (Flat File) kwa ajili ya kutunzia taarifa za Mwanafunzi kama Kiambatanisho A, B, C na ripoti za maendeleo yake shuleni.
10. Vitabu viwili vya kiingereza (Mali ya mwanafunzi)
    (i). Mabala the Farmer (ii). Hawa the Bus Driver
11. Vitabu vya kiada (Textbook) zilizo andikwa na **Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE)** kwa masomo yote anayosoma kidato cha kwanza.

**MAELEZO YA SARE YA SHULE: -**
**WAVULANA**

- Shati jeupe la mikono mifupi lisilo bana lenye **nembo** ya shule ya Mpiji Magohe.
- Suruali ya rangi **DARK BLUE (Rangi ya Kitambaa imeambatanishwa)** yenye upana wa cm 18 chini na marinda mawili kila upande.
- Tai ya rangi ya **DARK BLUE (Estim No 1).**
- Soksi ya rangi **NYEUSI**
- Viatu **vyeusi vya ngozi** visivyo na **kisigino kirefu** vya kufunga na **KAMBA matundu 3**
- Nywele fupi sio kipara.

**WASICHANA**

- Shati jeupe la mikono mifupi lisilo bana lenye **nembo** ya shule ya Mpiji Magohe.
- Sketi ya **MARINDA BOX RANGI DARK BLUE (Estim No 1). (Rangi ya Kitambaa imeambatanishwa)** isiyo na belt kubwa lisilozidi inch 2.
- Soksi ndefu za rangi nyeupe.
- Tai ya rangi ya **DARK BLUE** kwa wanafunzi wasiovaa JUBA.
- Viatu **vyeusi vya ngozi** visivyo vya **kisigino** vya kufunga na **Kamba matundu 3 au vya Juma na Roza (Visiwe Bajaji)**
- Nywele fupi sio kipara.

**SHERIA ZA SHULE; Nidhamu kwa ujumla (MWANAFUNZI ASOME VIZURI NA KUELEWA SEHEMU HII)**

1. Ni lazima mwanafunzi awahi shuleni asubuhi saa 1:00 na kufanya usafi wa mazingira ya shule na kuhudhuria gwaride la ukaguzi wa usafi na kuchangamsha mwili.
2. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kuondoka katika eneo la shule bila kupata kibali kutoka kwa mwalimu wa darasa, wa zamu au idara ya malezi.
3. Mwanafunzi anatakiwa kusimama, kusalimia na kuwapokea mzigo walimu au mtu yeyote mwenye umri mkubwa zaidi yake popote pale akutanapo na watu wa aina hiyo.
4. Hairuhusiwi kutumia **LUGHA CHAFU** miongoni mwa wanafunzi na kwa mtu mwingine yeyote.
5. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wanafunzi wenzake, viranja na wafanyakazi wote wa shule.
6. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya darasani na shughuli za michezo, na uzalishaji mali kwa mujibu wa ratiba.
7. Mwanafunzi lazima afanye mitihani ya masomo yote anayosoma shuleni hapa.
8. Mwanafunzi awapo shuleni haruhusiwi kuwa na aina yoyote ya vitu vifuatavyo:-
   Kucha ndefu, kupaka rangi, kuvaa cheni, hereni, nywele ndefu, kunyoa kipara, kunyoa nyusi, kupaka dawa nywele n.k.
9. Mwanafunzi ahakikishe kuwa awapo mahali popote ndani au nje ya shule awe amevaa nguo za heshima. Ni marufuku kuvaa nguo zinazobana, fupi na nyepesi.
10. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo zaidi ya zile zilizotajwa katika maelezo ya kujiunga na shule, ikiwemo sweta la rangi inayotakiwa.
11. Wanafunzi wanatakiwa kutunza mali zao binafsi na mali za shule. Pia wanatakiwa kutoa taarifa kwenye utawala juu ya uharibifu wa mali ya shule.
12. Ni marufuku kwa mwanafunzi yoyote kwenda kwenye maeneo yafuatayo bila sababu maalumu au bila kupewa ruhusa:-
    (i) Shule za jirani na madukani
    (ii) Nyumba zinazozunguka shule
    (iii) Vibanda vya biashara nje ya shule
13. Ni marufuku kwa mwanafunzi kukutwa sehemu zifuatazo:-
    (i) Baa na klabu za usiku
    (ii) Nyumba za kulala wageni isipokuwa wanapokuwa na wazazi au walezi wao
14. Wawapo shuleni wanafunzi hawaruhusiwi kumiliki vitu vya gharama kama: simu ya mkononi, redio, kamera, ipad, albam za picha na CD.
15. Kila mwanafunzi ni lazima afanye bidii katika kila somo. Mwanafunzi ambaye atapata chini ya 50% mwisho wa mwaka atakariri darasa (atarudia)
16. Hakikisha ukimya wa hali ya juu unazingatiwa katika maeneo yote ya shule naya kujifunzia hasa darasani, maktaba, maabara na kwenye korido wakati wa vipindi.
17. Adhabu ya viboko itaruhusiwa kwa kosa linalostahili na kuwa na taarifa/kibali cha Mkuu wa shule.
18. Hakikisha muda wote unapokuwa shuleni unaongea lugha ya Kiingereza nje na ndani ya darasa.
19. Mwanafunzi yeyote akikamatwa na kitu chochote kisichotakiwa shuleni kitaharibiwa mbele yake.

**B. MAKOSA AMBAYO MWANAFUNZI AKIYAFANYA ANAWEZA KUFUKUZWA SHULE**

1. Kutochukuwa ripoti ya maendeleo yake ya nusu mwaka au mwaka.
2. Ulevi au matumizi ya madawa ya kulevya.
3. Aina zote za wizi na unyang'anyi.
4. Aina zote za makosa ya kujamiiana na uasherati. Hii ni pamoja na kukutwa na mikanda ya video, vitabu vichafu vya uasherati au vitu vinavyofanana na hivyo.
5. Kupiga au kupagana.
6. Matumizi ya lugha chafu au matusi.
7. Makosa ya jinai.
8. Kuzomea watumishi au kuchokoza wanafunzi wengine.
9. Kugoma au kuchochea mgomo (ghasia).

10. Kutohudhuria shuleni kwa muda wa siku 30 mfululizo bila taarifa.
11. Kudharau Bendera ya Taifa kwa kutohudhuria paredi.
12. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule, (Pia ikithibitika kutoa mimba)
13. Kuoa au kuolewa.
14. Kukuwadia mwanafunzi mwenzie na mtumishi yeyote katika mambo ya mapenzi ndani na nje ya shule.
15. Kunyanyasa mwanafunzi mwenzie kutokana na jinsia yake, udini, ulemavu, ugeni wake au hali yake.
16. Kughushi mitihani au wizi wa mitihani, kukataa au kutofanya mitihani na mazoezi ya masomo bila sababu za msingi.
17. Kukataa adhabu kwa makusudi. Pia adhabu inaweza kutolewa na mwalimu au kiranja yeyote kwa mwanafunzi anayeonesha utovu wa nidhamu.
18. Kuharibu mali ya shule ikiwa ni pamoja na majengo, mali ya mtu au kundi la watu.
19. Kukamatwa na simu, redio kamera, ipad, albam za picha na CD kwa mara ya pili baada ya kuonywa kwa mara ya kwanza.

**C. WAJIBU WA MZAZI**

1. Mzazi/Mlezi anatakiwa kumleta mwanae kumwandikisha shuleni anapoanza masomo.
2. Mzazi/Mlezi anatakiwa kuandikisha majina ya watu wanne na namba zao za simu watakoruhusiwa kupata ripoti za mtoto akiwa shuleni. Mzazi/mlezi anawajibika kutoa taarifa ya **mabadiliko ya namba za simu** kwa uongozi wa shule.
3. Mzazi/Mlezi anatakiwa kuja kuchukuwa ripoti ya mtoto wake kwa muhula husika vinginevyo hatapokelewa muhula unaofuata.
4. Mzazi/Mlezi anatakiwa kufika shuleni kwa muda muafaka pindi anapohitajika na uongozi wa shule.
5. Mzazi/Mlezi ajenge tabia ya kutembelea shule mara kwa mara ili kujua maendeleo ya mtoto wake badala ya kusubiri kuitwa ili kujenga mshikamano wa malezi.
6. Mzazi/Mlezi amfahamu kwa jina na namba ya simu mwalimu wa darasa la mtoto wake ili kujenga mahusiano ya malezi ya mtoto.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU.**

**………………………………**

**MKUU WA SHULE**

**MUHIMU:**

**Fomu zilizoambatanishwa zinatakiwa zijazwe kikamilifu na zirudishwe shuleni.**

1. Fomu rasmi ya kuandikishwa.
2. Ahada ya mwanafunzi na Mzazi/Mlezi.
3. Fomu ya uchunguzi wa Daktari.

**KIAMBATISHO 'A'**
**FOMU RASMI YA KUANDIKISHWA**

**Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi:-**

PICHA YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi: ……………………………………………………..
2. Uraia: …………………………………………………………………………
3. Dini: …………………………………………………………………………..
4. Tarehe ya kuzaliwa: …………………………………………………………
5. Mahali ulipozaliwa (**Wilaya**): …………………………………………………
6. Yatima/Sio yatima/Mzazi mmoja (kata isiyohusika)
7. Shule uliyosoma kabla ya kuja **Makabe sekondari** (Jaza jedwali)

| MAJINA MATATU YALIYOANDIKISHWA SHULENI | SHULE YA MSINGI ULIKOTOKA | MWAKA ULIOANZIA | MWAKA ULIOTOKA |
|---|---|---|---|
| | | | |

**KAMA NI MUHAMIAJI**

| SHULE YA SEKONDARI ULIYOTOKA | WILAYA ILIYOPO | MKOA | KIDATO ULICHOHAMIA | TAREHE YA KUHAMIA |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

**Saini ya mwanafunzi:** …………………………………………..... **Tarehe:** ………………………………

Sehemu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi:

PICHA YA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi: ………………………………………………….
2. Uraia: ……………………………………………………………………….
3. Anuani kamili mjini DSM: ………………………………………………..
4. Sehemu unayoishi Wilaya: ……………………………………………......
5. Mtaa: ………………………………………………………………………
6. Kata: ………………………………………………………………………..
7. Namba ya Simu: (baba/mlezi)…………………………………………………
8. Namba ya Simu: (mama/mlezi)………………………………………………..
9. Kazi anayofanya mzazi/mlezi…………………………………………………. (Mf: Karani, Meneja n.k)

Ndugu wengine wa

| S/N | JINA LA NDUGU | ANAPOISHI | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |

**Saini ya Mzazi/Mlezi:** ………………………………………….. **Tarehe:** ………………………

**KIAMBATANISHO “B”**

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………………………………………….. **(Majina matatu)**

1. Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote na nimekubali kujiunga na shule ya Sekondari Makabe kuanzia tarehe ………………………………………………………………………...
2. **Naahidi kwamba:-**
   a) Nitazingatia Sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.
   b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
   c) Nitatunza mali ya Umma ambayo ni pamoja na Majengo, Samani, Vitabu na vifaa vya Maabara.
   d) Nipo tayari kuchukuliwa hatua yoyote stahiki endapo nitakiuka malekezo yaliyotolewa kwenye fomu hii.

Saini ya Mwanafunzi: ………………………………… Tarehe: ……………………………

---

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………… Kidato cha ………Mwaka……………

Na ahadi kwamba:-

1. Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule na walimu wote kwa ujumla katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii ni kuhakikisha kuwa atazitii Sheria zote za shule na kuyazingatia mambo yote muhimu yaliyotajwa.
2. Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kufika shuleni kila siku kabla ya saa 1:00 asubuhi.
3. Na kwamba mwanafunzi atahitimu na kufuzu Kidato cha Kwanza hadi cha Nne.
4. Ninaruhusu mwanangu achukuliwe hatua yoyote stahiki endapo atavunja mojawapo ya sheria na Kanuni zilizoorodheshwa.

Saini ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………. Tarehe: …………………………..

**MAKABE SECONDARY SCHOOL**

**P.O.BOX ……………**

**DAR ES SALAAM**

**A RECOGNISED MEDICAL DOCTOR MUST FILL THIS FORM**

To the Medical Officer

………………………………Hospital

………………………………

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:**

Please examine………………………………………………………… **(Name of student)** who has been selected to join this school. Please comment on his/her fitness as a student in the following areas:-

1. Eye sight……………………………………………………………………………………………

2. Hearing…………………………………………………………………………………………...

   Specimens:

   a) Urine……………………………………………………………………………………

   b) Blood……………………………………………………………………………………

   c) Stool……………………………………………………………………………………

3. Asthma…………………………………………………………………………………………

4. Tuberculosis…………………………………………………………………………………

5. Pregnancy……………………………………………………………………………………

6. Others…………………………………………………………………………………………

**COMMENTS:**

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE:** (To be completed by Medical Doctor)
I ………………………………………………………………. **(Name of the Medical Doctor)** have examined the above and considered that he/she is fit/ not fit as a student.

**Signature**………………………………………............................**Designation**…………………………

**Official stamp**……………………………………………………**Date**……………………………………